

HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA



MWALIKO WA ZABUNI

ZABUNI YA UPANGISHAJI WA MAENEO YA BIASHARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

ZABUNI NAMBA LGA/003/2020/2021/NC/01

1. Halmashauri ya Jiji la Arusha inapenda kuwaalika watu binafsi, makampuni, Ushirika, Taasisi au vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria vyenye nia ya kuwa wapangaji katika maeneo ya biashara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama ifuatavyo:-

SEHEMU/ENEO	CHUMBA NAMBA	
Krokoni	ACC/KR/...	01,02,03,04,05,06,07,08,09,10,11,12,13,14,15, 16,17,18,19,20,21,22,23,24 na 25
Ranger Safari	ACC/RS/....	50,51,52,53,54,55,56,57,58,59,60,61,62,63,64, 65,66,67,68,69,70,71,72,73,74,75,76 na 77
Kata ya Kati	ACC/VK/...	06

2. Maombi yote ya zabuni yazingatie masharti yafuatayo
 - i) Maombi ya zabuni yaambatanishwe na nakala ya malipo ya Tshs. 50,000/= (Elfu hamsini tu) kupitia akaunti ya Halmashauri ya Jiji la Arusha iliyopo katika Benki ya NMB tawi la Clock Tower. Akaunti Na. 40801200336 baada ya kupatiwa control number ya malipo na kuwasilisha nakala ya hati ya malipo ya Benki (Bank Pay in slip Original) na kupata stakabadhi ya Halmashauri kwa zabuni iliyoombwa. Malipo yaliyotolewa kwa ajili ya maombi hayo hayatarejeshwa.
 - ii) Zingatia kuwa fomu ya maombi ya Zabuni pamoja na nyaraka nyingine za zabuni zitajazwa na kusainiwa na mwenye uhalali wa kisheria (power of Attorney/ Affidavit), ambayo lazima iambatanishwe katika zabuni hii

- iii) Mwombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri, asiwe na historia ya kusababisha migogoro na wala asiombe kwa nia ya kumpangishia mtu mwingine chumba.
 - iv) Maombi yote yaambatanishwe na kiapo dhidi ya vitendo vya Rushwa.
 - v) Mwombaji lazima awe na leseni hai ya biashara pamoja na TIN.
 - vi) Kampuni lazima ziambatanishe hati ya usajili wa kampuni, wasifu wa kampuni pamoja na orodha ya wamiliki.
3. Mwombaji atakayeshindwa kutimiza masharti ya zabuni hii atakuwa amejiondoa mwenyewe kwenye mchakato mzima wa zabuni.
 4. Waombaji wote wenye nia na uwezo wanaweza kupata taarifa kamili kuhusiana na maeneo hayo kwa Afisa Biashara wa Jiji la Arusha S.L.P 3013 Arusha kila siku kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 mchana, siku za Jumatatu hadi Ijumaa, ukiondoa siku za sikukuu zinazotambulika Kitaifa, kuanzia tarehe ya tangazo hili.
 5. Maombi yote yawekwe katika bahasha na kufungwa kwa lakiri (Seal) bila ya kuonesha inatoka wapi na juu yake iandikwe kwa herufi kubwa Original na Copy, Eneo la chumba kinapooombwa na namba ya chumba yatumwe kwa Mkurugenzi wa Jiji la Arusha. S.L.P 3013 Arusha na kutumbukizwa katika sanduku la Zabuni lililopo katika Ofisi ya Manunuzi (chumba Na. 66) Ofisi Kuu ya Halmashauri ya Jiji la Arusha.
 6. Mwisho wa kupokea Zabuni ni saa nne kamili (4:00) asubuhi ya tarehe 19/05/2020 katika ofisi za Halmashauri ya Jiji la Arusha zilizopo Barabara ya Boma. Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa kushuhudia ufunguzi. Ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea zabuni. Waombaji au wawakilishi wasiozidi kumi wataruhusiwa kuhudhuria ufunguzi huo. (Hii ikiwa ni mojawapo ya njia madhubuti za kukabiliana na maambukizi ya virusi vya COVID 19 vinavyosababisha homa kali ya mapafu (CORONA))
 7. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa hazitapokelewa.
 8. Maelekezo yote yaliyotolewa katika tangazo hili pamoja na yale yaliyoko katika nyaraka za maombi ya zabuni ni sehemu ya masharti kwa mwombaji zabuni.

Dr. Maulid S. Madeni (PhD)
**MKURUGENZI WA JIJI
ARUSHA**

